SHULE YA SEKONDARI MISIMA,
S. L. P 192,
HANDENI - TANGA,
11/04/2022.

Namba za simu

The Head Master: 0719029733/068503733/0743818151.

Second Master: 0677671520

Academic Master: 0755015247

Mzazi/ Mlezi wa……..……

S. L.P……..

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MISIMA HALMASHAURI YA MJI HANDENI MKOA WA TANGA MWAKA 2022/2023.

1. UTANGULIZI

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2022/2023 tahasusi ya CBG/PCB (kata isiyohusika)

Shule ya Sekondari MISIMA ni shule ya Serikali ya mchanganyiko kwa Kidato I-IV ambao ni wa kutwa na ni ya Wasichana kwa vidato V-VI (mchepuo wa sayansi- CBG/PCB) ambao ni wa Bweni. Na ipo umbali wa kilometa 21 kutoka Halmashauri ya Mji Handeni.

2. NAMNA YA KUFIKA SHULENI

Unaweza kufika shuleni kupitia mojawapo ya njia zifuatazo:-

- **Ukitokea Tanga mjini**; panda mabasi ya Tanga – Korogwe – Handeni. Shuka Misima (nauli sh.6000). Panda pikipiki waambie wakupeleke MISIMA Sekondari (nauli sh. 2,000).

- **Ukitokea Dar es Salaam**; panda basi la **Dar – Handeni** (Stendi ya Magufuli (Mbezi) ndani nauli sh. 14,000/=). Shuka stendi ya Chogo Handeni Mjini. Panda gari zinaoelekea KOROGWE, shuka MISIMA (nauli sh. 2,000). Panda pikipiki waambie wakupeleke MISIMA Sekondari (nauli sh. 2,000).

- Ukitokea mikoa mingine kwa mfano **Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Singida** na kwingineko **mikoa ya kaskazini** Shuka stendi ya Korogwe. Ulizia gari za kwenda Handeni Shuka Misima (nauli sh.3000). Panda pikipiki waambie wakupeleke MISIMA Sekondari (nauli sh. 2,000).

  NB: Kama umepanda basi la Hajees/ KSK/ Mapenzi ya Mungu na mengineyo ya moja kwa moja Kutoka Arusha hadi Handeni. Shuka Misima. Panda pikipiki waambie wakupeleke MISIMA Sekondari (nauli sh. 2,000).

3. MUHULA WA MASOMO

Muhula wa masomo unaanza tarehe 04/07/2022. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 12/07/2022. Mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe 30/07/2022.

NB: Ukichelewa nafasi yako itachukuliwa na mwanafunzi mwingine.

4. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

4.1 **Sare ya shule:**

a) Sketi mbili Damu ya mzee (Maroon) mshono Rinda box. – 35,000/ (Zinapatikana Shuleni).
b) Mashati mawili meupe mikono mirefu.
c) Tai (Damu ya mzee/ Maroon).
d) Sweta (Nyeusi).
e) T- Shirt moja (Blue) - 10,000/= (Zinapatikana shuleni).
f) Hijabu nyeupe (Tetron).
g) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
h) Soksi jozi mbili nyeupe au zaidi.
i) Raba nyeusi/nyeupe (kwa ajili ya michezo).
j) Nguo za michezo ni track-suit rangi nyeusi (yenye ufito mweupe pembeni) na fulana (t-shirt nyeupe) isiyo na maandishi wala michoro.
k) Nguo za kushindia (shamba dress) ni gauni rangi ya kijivu mshono wa solo,kwa wanaovaa hijab shamba dress yao itakuwa ni juba la mpira rangi ya kijivu.

MALAZI:

(i) Shuka mbili za pink (plain)
(ii) Mto na foronya
(iii) Godoro la futi 2½, unene nchi 4
(iv) Chandarua 1 cheupe
(v) Blanket nyepesi
(vi) Ndoo 1 (ya lita 20), na ndoo 2 (za lita 10)

VYOMBO VYA CHAKULA:

(i) Sahani
(ii) Kijiko
(iii) Kikombe
(iv) Bakuli

MAHITAJI MENGINE:

(i) Mwamvuli/ Koti la mvua
(ii) Taulo
(iii) Malapa
(iv) Mswaki
(v) Kanga mbili au vitenge 2
(vi) Nguo ya kulalia na mahitaji mengine ya mtoto wa kike.
(vii) Taa ya solar (itatumika wakati umeme ukikatika).

VIFAA VYA USAFI:

(i) Jembe lenye mpini (Wanafunzi Wote)

(ii) Mopper na squeezer (Wanafunzi Wote)

(iii) Hard broom (Wanafunzi wa CBG)

(iv) Soft broom (Wanafunzi wa PCB)

VIFAA VYA TAALUMA: (Anavyotakiwa kuja navyo)

i. Daftari zisizopungua 10.

ii. Kalamu za kutosha.

iii. Mkebe wa mahesabu.

iv. Rimu (1) ya karatasi nyeupe A4, Ruled paper rimu (1) na vitabu vya mchepuo wake.

v. Dissecting kit kwa wanafunzi wa somo la Biolojia **(ITAKAGULIWA).**

vi. Non Programmable Scientific calculator kwa wanafunzi wa tahasusi za **CBG na PCB (ITAKAGULIWA).**

vii. Stop watch kwa wanafunzi wa tahasusi za **CBG na PCB (ITAKAGULIWA**).

4.2 **ADA NA MICHANGO MINGINE**

a) Ada ya shule kwa mwaka ni sh.70,000/= unaweza kulipa kiasi cha sh 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na. **41401200054** katika benki ya **NMB**: Jina la **Account MISIMA Secondary School** (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye benki **pay-in-slip** na aje nayo shuleni na nakala halisi siku ya kuripoti)

b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

MAHITAJI	**GHARAMA**
Taaluma	20,000/=
Ukarabati wa samani	15,000/=
Kitambulisho na picha	6,000/=
Wapishi, walinzi na vibarua wengine.	30,000/=
Nembo ya shule.	2,000/=
Huduma ya kwanza. (Mwenye Bima ya Afya aje nayo)	20,000/=
Mitihani ya mock (atalipa akiwa kidato cha sita)	25,000/=
Tahadhari.	10000/=
Mahafali (atalipa akiwa kidato cha sita).	20,000/=
Dawati	15,000/=
JUMLA	**163,000/=**

JUMLA ya michango hiyo yote ni shilingi **163,000/=** kwa mwaka.

NB: 1. Michango hii iwekwe benki ya NMB Account Na. : **41402300584** Jina la Account **MFUKO WA SHULE, MISIMA SHULE YA SEKONDARI.**

2 (Mwanafunzi aje na nakala halisi za malipo ya Benki (Bank **pay-in-slip**) zote mbili zikiwa zimeandikwa majina halisi la mwanafunzi).

3. Tunaomba Ada na Michango mengine ianze kuingizwa kuanzia tarehe **01/07/2022**.

4. **Mwanafunzi aje na nakala ya "Result slip" ya kidato cha nne na nakala ya cheti cha kuzaliwa.**

5. SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE

Shule ya sekondari MISIMA ni shule ya serikali hivyo inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na maelekezo mbalimbali yanayotolewa na serikali. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
(c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (prep.)
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(i) Mwanafunzi atakapofika shuleni awe amekata nywele robo nchi na zisiwe zimewekwa dawa. Shuleni hakuna kusuka nywele.
(j) Hereni, bangili, vipini, kofia, miwani ya jua, mikufu na pete za aina yoyote havitarusiwa kuvaliwa shuleni.
(k) Ni marufuku kumruhusu mgeni kufika eneo la mabweni na kuingia mabwenini. Hivyo basi mwanafunzi haruhusiwi kuongea au kupiga gumzo na mtu yeyote asiyekuwa mwanajumiaya wa shule hii katika eneo lolote la Shule bila kibali cha mwalimu wa zamu. Kwa hiyo mwanafunzi haruhusiwi kukaribisha au kupokea mgeni wake nje ya utaratibu wa shule.
(l) Ni marufuku mwanafunzi wa shule hii kuwa na simu ya mkononi. Mawasiliano kati ya wazazi/mlezi yatafanyika kupitia ofisi ya Mkuu wa Shule kwa simu zilizooneshwa kwenye ukurasa wa kwanza.
(m) Ni lazima mwanafunzi wa kidato cha tano na sita akae Bweni

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule

a. Wizi
b. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
c. Kutoa lugha Chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
d. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
e. Uasherati, ushoga na usagaji.
f. Ubakaji Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, uvutaji wa Sigara, Cocaine, mirungi, kuberi n.k.
g. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
h. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
i. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
j. Kudharau bendera ya Taifa na nembo za taifa kwa ujumla.
k. Kuolewa.
l. Kupata mimba, kutoa mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
m. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
n. Kukataa adhabu kwa makusudi
o. Mwanafunzi kumiliki simu ya mkononi, redio na pasi ya umeme au kifaa chochote kinachotumia umeme.
p. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

5.2 Sehemu zifuatazo zitatembelewa kwa ruhusa maalumu:

- Nyumba za walimu
- Hospitali na kwenye nyumba za ibada
- Maduka ya mjini(MISIMA/ HANDENI MJINI na Miji mingine ya jirani)
- Jengo la utawala
- Ukumbi wa walimu (staff room)

6 MAHUDHURIO:

6.1 Kila mwanafunzi lazima ahudhurie pale anapotakiwa bila kukosa wala kuchelewa.

6.2 Ni lazima mwanafunzi awepo shuleni muda wote wa masomo

6.3 Ni lazima mwanafunzi awahi na kushiriki katika shughuli zote za shule kama kuitwa majina 'Roll Call'

6.4 Ruhusa ya kuondoka shuleni kwa ajili ya shida nzito kama msiba itatolewa na Mkuu wa Shule au makamu wake iwapo atakuwa hayupo Mkuu wa Shule.

6.5 Ruhusa ya kwenda Hospitali itatolewa na Matron wa shule baada ya kumwona mwanafunzi mgonjwa akishirikiana na mwalimu wa zamu.

6.6 Mzazi/mlezi aliyeandikishwa shuleni ndie anayeruhusiwa kumwombea mwanafunzi ruhusa kila itakapolazimika kufanya hivyo na siyo vinginevyo.

7 UVAAJI WA SARE ZA SHULE NA UNADHIFU :

7.1 Wakati wote mwanafunzi awapo darasani anatakiwa kuvalia sketi ya Damu ya Mzee (Maroon) (Rindabox), shati nyeupe ya mikono mirefu na tai Damu ya Mzee (Maroon). Kwa wanaovaa hijab wavae juba jeupe linalofika kwenye magoti na sketi ndefu ya rangi ya Damu ya Mzee (Maroon).

7.2 Baada ya muda wa masomo, mwanafunzi atavalia shamba dress.

7.3 Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele.

NB: 1. Siku za kutembelea wanafunzi (visiting days) ni kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi.

2. Shule haitatoa huduma ya "Special Diety" (Mlo maalum) kwa wenye matatizo. Mf Vidonda vya tumbo n.k

8. **MWISHO**:

Hakikisha unafika shuleni tarehe iliyopangwa. Usipo fanya hivyo, wala kutoa taarifa ya kutofika utahesabiwa kuwa hutafika na nafasi itarudishwa katika mamlaka husika za uchaguzi ili nafasi hiyo wazi iweze kuchukuliwa na mwanafunzi mwingine. Mzazi/mlezi una wajibu wa kumpatia mwanao **fedha za kujikimu** awapo shuleni pamoja na **nauli** ya kwenda na kurudi wakati wa likizo au kwa dharura yoyote.

Ninachukua nafasi hii kukukaribisha tena MISIMA Sekondari na ni matarajio yangu kuwa utaitumia vyema nafasi hii uliyotunukiwa na Taifa lako.

KARIBUNI SANA MISIMA SEKONDARI

……

STANSLAUS M. KOVAGA

(Mkuu wa Shule)

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI MISIMA

A: **TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**:

i) JINA LA MWANAFUNZI ……

ii) TAREHE YA KUZALIWA ……

iii) MAHALI ULIPO ZALIWA (MKOA/WILAYA) ……

iv) UNAISHI/UNAKAA WAPI (MKOA/WILAYA)……

v) URAIA …….

vi) SHULE ULIYOTOKA …….

vii) NAMBA YA MTIHANI ……

B: **TAARIFA YA MZAZI:**

i) JINA LA MZAZI/MLEZI

……..

ii) KAZI YA MZAZI/MLEZI ……

iii) ANUANI YA MZAZI/MLEZI ……..

iv) SIMU YA MZAZI/MLEZI: KAZINI ……...

v) NYUMBANI …… MKONONI ……..……

vi) MAHALI ANAPOKAA/KUISHI MZAZI/MLEZI (MKOA/WILAYA)…….

C: **KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA**:

Mimi ……. Kidato …… mwaka …….. Nimesoma na nakuyaelewa yote. Kwa hiyo nakubali /sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimepokea maagizo au maelekezo bila kulazimishwa na nitayazingatia.

Tarehe …… Sahihi ……

D**: KUKUBALI SHERIA ZA SHULE:/ MWANAFUNZI**.

Mimi ……. Nimezisoma na kuzielewa sheria za shule na naahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti, sheria za shule na maelekezo mengine nitakayo pewa na walimu wote wa shule, nikikiuka sheria hizo hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Tarehe …….. Sahihi ……

FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKIRI KUKUBALI KULIPA ADA/MICHANGO NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE

E: **MAZAZI/ MLEZI** – (ajaze sehemu hii)

i. Mimi …….ambaye ni Mzazi/mlezi, nathibitisha kuwa mwanangu ……..……jina la (mtoto) ameelewa maagizo ninapenda ifahamike kuwa dini ya mwanagu ni …… dhehebu lake ni ……

ii. Ninaruhusu/siruhusu (kata isiyohusika) mwanangu kushiriki katika makongamano au warsha za kidini nje ya shule zinazofanyika nje na ndani ya mkoa wa Tanga zitakazo fanyika kwa ruhusa ya mkuu wa shule hii.

iii. Nimeruhusu/ siruhusu (kata isiyohusika) wakati wa likizo fupi (mid term) mwanangu atoke shuleni na kwenda kwa ……..…… wa (mahali) …… uhusiano wake na mwanangu ni …… namba yake ya simu ni ……

iv. Aidha, mimi …….…….. ambaye ni mzazi/mlezi, nimesoma/ nimesomewa sheria na maagizo mengine ya shule yanayohusu mwanafunzi (jina la mwanafunzi) ……naahidi kutimiza wajibu wangu nikiwa mzazi/mlezi wa mtoto huyu kwa kumshauri ipasavyo pamoja na kumtimizia mahitaji yake ya shule.

v. Picha nne za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

JINA LA MZAZI /MLEZI	NDUGU 1	NDUGU 2	NDUGU 3
……..	……	……	…….
SIMU……	…….	…….	……
UHUSIANO…….	……..	……..	……

…….…… …….. ……

JINA LA MZAZI/MLEZI SAHIHI TAREHE

NJOO NA VITABU VYA COMBINATION YAKO MUHIMU SANA

GEOGRAPHY

1. Human and Economic Geography by Goh Ching Leong & Gillian C Morgan (2nd Edition)
2. Certificate Physical and Human Geography by Goh Ching Leong (3rd Edition)
3. Principle of Physical Geography by F. Monk house (2000)
4. Practical Geography of Africa by Prichard j, M. (1976)

GENERAL STUDIES - (a) A level General studies Notes

CHEMISTRY

1. General Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Student's Book, Form Five and Six (TIE)
2. Physical Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Student's Book, Form Five and Six (TIE)
3. Organic Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Student's Book, Form Five and Six (TIE)
4. Inorganic Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Student's Book, Form Five and Six (TIE)

BIOLOGY

1. Biology Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Student's Book, Form Five (TIE)
2. Biology Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Student's Book, Form Six (TIE)

PHYSICS

1. Principles of Physics Chand (1&2)
2. Nelkon and Park (7th Edition)

BASIC APPLIED MATHEMATICS

- Basic Applied Mathematics Form five and six by TIE (2019)

N. B. VITABU HIVYO NI MALI YA MWANAFUNZI

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A

The Head Master,

MISIMA Secondary School,

P. o. Box 192,

Handeni – Tanga.

TO,

The Medical office,

……

……

…….

…….(Name of student in full) please examine the above mentioned student as to her physical and mental fitness for a full time student. The examination should include the following category (a- c)

a. (i). Eyesight (ii) Hearing (iii) Speech (iv) Venereal disease

(v) Limbs

b. Neurosis

c. Other serious diseases eg. Asthma, Tb etc

Name …… Date ……..signature ……

PART B: MEDICAL CERTIFICATE

(to be completed by a Government Medical Officer) I have examined the above student and consider that she is fit/unfit full time studies.

i. Eyesight …….
ii. Hearing ……
iii. Speech ……..
iv. Limbs ……
v. Venereal diseases ……
vi. Leprosy …….
vii. Epilepsy …….
viii. Neurosis …….
ix. T.B …….
x. Other serious disease e.g. Asthma …….

Other Comments ……

Name …… Date …… Signature ……

STATION …….. DESIGNATION ……..

Official stamp……..